

**HOTUBA YA MHE. SAMIA SULUHU HASSAN,
RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA
TANZANIA, KWENYE HAFLA YA UZINDUZI WA
KITABU CHA HISTORIA YA MAISHA (TAWASIFU)
YA MHESHIMIWA MZEE ALI HASSAN MWINYI,
RAIS MSTAAFU WA AWAMU YA PILI YA JAMHURI
YA MUUNGANO WA TANZANIA
DAR ES SALAAM, TAREHE 8 MEI, 2021**

*Mheshimiwa Mzee Ali Hassan Mwinyi, Rais Mstaafu
wa Awamu ya Pili wa Jamhuri ya Muungano wa
Tanzania na Mheshimiwa Mama Siti Mwinyi;*

*Mheshimiwa Mzee Jakaya Mrisho Kikwete, Rais
Mstaafu wa Awamu ya Nne wa Jamhuri ya
Muungano wa Tanzania;*

Mheshimiwa Philip Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Waheshimiwa Makamu wa Rais Wastaafu mliopo;

Mheshimiwa Dkt. Hussein Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi pamoja Marais Wastaafu wa Zanzibar mliopo;

Mheshimiwa Kassim Majaliwa (Mb), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mawaziri Wakuu Wastaafu mliopo;

Mheshimiwa Job Ndugai, Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na Waheshimiwa Maspika Wastaafu mliopo;

Mheshimiwa Prof. Ibrahim Juma, Jaji Mkuu wa Tanzania n;

Ndugu Makamu Wenyeviti wa CCM Tanzania Bara na Zanzibar

Waheshimiwa Mawaziri mliopo;

Waheshimiwa Wabunge mliopo;

*Mheshimiwa Balozi Hussein Kattanga,
Katibu Mkuu Kiongozi;*

*Mheshimiwa Abubakar Kunenge, Mkuu wa Mkoa
wa Dar es Salaam;*

*Waheshimiwa Mabalazi na Wawakilishi wa Taasisi za
Kimataifa, akiwemo Mwakilishi wa Ubalazi wa
Finland;*

*Ndugu Makatibu Wakuu na Viongozi wengine wa
Serikali mliopo;*

*Wakuu wa Vyombo vya Ulinzi na Usalama wa Sasa na
Wastaafu mliopo;*

Viongozi wa Taasisi ya Uongozi;

*Waheshimiwa Viongozi wa Vyama vya Siasa na Dini
mliopo;*

Waheshimiwa Wageni wote Waalikwa;

Ndugu Wana-habari, Mabibi na Mabwana:

**NAWASALIMU KWA JINA LA MUUNGANO
WA TANZANIA**

Nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema, aliyetujalia uhai na kutuwezesha kukutana hapa leo tukiwa wenye afya njema. Aidha, namshukuru sana Mzee wangu, Mheshimiwa Ali Hassan Mwinyi, Rais Mstaafu wa Awamu ya Pili wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kunialika kwenye tukio hili adhimu la Uzinduzi wa Kitabu kinachoelezea Historia ya Maisha

yake alichokipa jina la *“Mzee Rukhsa: Safari ya Maisha Yangu”*. Ahsante sana Mzee wangu.

Kama ulivyoeleza kwenye Hotuba yako, shughuli ya uzinduzi wa Kitabu hiki ilipangwa ifanywe na Mtangulizi wangu, Hayati Rais Dkt. John Pombe Joseph Magufuli mwezi Machi mwaka huu. Hata hivyo, kwa mapenzi ya Mungu, hakuwahi kuifanya kazi hiyo. Hivyo basi, tuendeleo kumwomba kwa Mwenyezi Mungu aipumzishe roho yake mahali pema peponi. Amin.

Napenda pia kutumia fursa hii, hapa mwanzoni kabisa, kukupongeza sana Mzee Mwinyi kwa kuamua kuandika Kitabu hiki, ambacho sio tu kitawasaidia Watanzania na dunia kukufahamu wewe binafsi, kitabu hiki pia kina maelezo ya historia ya Taifa letu.

Nakupongeza pia kwa kuamua kuandika kitabu chako kwa lugha ya Kiswahili, lugha uliyoibobea na inayoeleweka na kutumiwa na Watanzania wengi. Hii, naamini, itawahamasisha Watanzania wengi kukitafuta na kukisoma. Aidha, Kitabu hiki kitasaidia kuonesha ufasaha wa lugha kama ilivyotumika humu. Kama ambavyo mwenyewe umeeleza *“sisi Tanzania ndiyo chemchem ama chimbuko la Kiswahili hivyo tunao wajibu mkubwa wa kukikuza, kukilinda na kukitangaza kimataifa”*. Kitabu hiki kina sifa zote hizo za kukikuza, kukilinda na kukitangaza Kiswahili.

Sambamba na kukienzi Kiswahili, nakushukuru Mzee Mwinyi kwenye Kitabu chako umetukumbusha Wosia wa Baba wa Taifa, Mwalimu Nyerere, kwa Watanzania kuhusu kutopuuzia lugha ya Kiingereza,

ambayo aliita **“Kiswahili cha Dunia”** alitoa wosia huo kwasababu Tanzania haiishi peke yake duniani, na hivyo, tutahitaji kushirikiana na dunia katika mambo mbali mbali. Nami niseme, kwa wakati huu tulionao, ni vyema kujifunza lugha kadhaa ambazo zimekubalika kutumika kama lugha za mawasiliano katika Jumuiya za Kikanda na Kimataifa. Lakini tusingahau, kutukuza kilicho chetu nacho kifikie hadhi hiyo.

Waheshimiwa Viongozi;

Wageni Waalikwa, Mabibi na Mabwana;

Kama ilivyoelezwa na Taasisi ya Uongozi, hafla hii ya uzinduzi wa Kitabu hiki inakwenda sambamba na Kumbukizi ya Siku ya Kuzaliwa ya Mzee Mwinyi. Hivyo basi, kwa niaba ya Serikali pamoja na Watanzania wote tunampongeza Mzee wetu Mwinyi kwa kutimiza miaka

96. Mwenyezi Mungu akujaalie umri Tawwil wenye Afya, Nguvu na Siha. Aamiin.

Tunafarijika sana kukuona ukiendelea kuwa mwenye afya njema, MashaAllah. Hii, bila shaka, inalisadifu jina lako la “Nzasa” (*isiyokauka*). Kwa ujumla, na jinsi nilivyokisoma Kitabu hiki, nimeiona kuna mengi yanayomfanya Mzee mwinyi awe hivyo alivyo, ikiwemo Ucha Mungu. Tunamwomba Mwenyezi Mungu atuwekee hazina yetu ili tuzidi kunufaika na nasaha zako, tufurahie ucheshi wako na pia tuvune hekima na busara zako.

Waheshimiwa Viongozi;

Wageni Waalikwa, Mabibi na Mabwana;

Hivi punde tumesikia Muhtasari wa Kitabu cha Mzee Mwinyi, *Mzee Rukhsa*, kutoka kwa Prof. Rwekaza

Mukandala. Mimi pia nimepata fursa ya kukisoma Kitabu hiki. Kimesheni mambo mengi sana. Kimeeleza historia ya Mzee Mwinyi tangu alipozaliwa Mkuranga tarehe 8 Mei, 1925 akiwa mtoto wa mwisho na wa pekee wa kiume kwa wazazi wake; kuhamia Zanzibar na kuanza Madrasa pamoja na Shule; kazi ya ualimu; kuingia Serikalini, Ubalozi, Uwaziri, Urais wa Zanzibar na hatimaye Urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hii ni safari ndefu, Hongera sana Baba yetu.

Zaidi ya hapo, Mzee Mwinyi ametupatia *Bonus* kwa kutenga sura tatu za mwanzo za Kitabu chake kueleza masuala ya kihistoria, hususan Visiwani Zanzibar. Anaeleza kwamba wakati wa Ukoloni, maisha yalikuwa magumu sana kwa Waafrika. jitihada za mwanzo za

Waafrika kudai uhuru zilianza miaka ya mwanzoni ya 1930; lakini zilikumbana na vikwazo mbalimbali kutoka kwa Watawala. Pamoja na kuwepo kwa vikwazo vingi, hatimaye tarehe 5 Februari, 1957, Chama cha *Afro Shiraz Party* (ASP), ambacho kiliongoza Wazanzibar kwenye Mapinduzi Matukufu ya Mwaka 1964 yaliyoleta Uhuru wa kweli Visiwani Zanzibar, kilianzishwa chini ya Uongozi wa Mzee Abeid Amani Karume. Cha kufurahisha zaidi ni kwamba, Mkutano wa kuanzisha ASP ulihudhuriwa na viongozi wakuu wa TANU, Mwenyekiti, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere na Katibu wake Mkuu, Zuberi Mtemvu. Na hii ni ishara kuwa uhusiano kati ya Tanganyika na Zanzibar ni wa kindugu na kihistoria; na Muungano wetu umejengwa katika misingi hiyo.

Waheshimiwa Viongozi, Mabibi na Mabwana;

Natamani nieleze yote yaliyomo kwenye Kitabu cha Mzee Mwinyi; lakini nachelea kufanya hivyo kwa vile nahofia nikifanya hivyo, Kitabu hiki kinaweza kukosa wanunuzi. Hivyo basi, itoshe tu kusema kuwa, kwa yeyote atayekisoma, atajifunza mambo mengi sana. Binafsi, nimepata mambo mengi ya kujifunza kama Kiongozi kupitia Kitabu hiki cha Mzee Mwinyi. Kubwa kuliko yote, na naamini Watanzania wengi watakubaliana na mimi ni kwamba, Mzee Mwinyi ni Baba wa Mageuzi nchini.

Yeye ndiye aliyesimamia mageuzi makubwa ya kiuchumi. Kwa watu wa umri wangu watakumbuka, na kwa bahati nzuri, Mzee Mwinyi mwenyewe ameeleza kwenye Kitabu chake kuwa, wakati anaingia

madarakani, hali ya uchumi wa nchi yetu ilikuwa mbaya sana kutokana na matatizo mbalimbali, ikiwemo kupanda kwa bei ya mafuta mwaka 1973, ukame wa mwaka 1975, kuvunjika kwa EAC, kuibuka kwa vita vya Tanzania na Uganda, pamoja na masharti magumu tuliyopewa na wafadhili na taasisi za kifedha za kimataifa mwanzoni mwa miaka ya 1980. Hii ilifanya nchi yetu kuwa na uhaba wa fedha za kigeni na kusababisha upatikanaji wa bidhaa muhimu, ikiwemo vyakula, mavazi, vipuri kuwa mgumu. Ilikuwa vigumu hata kupata dawa ya kusafishia meno. Nakumbuka wakati huo Zanzibar chakula kilikuwa kinatolewa kwa kuzingatia idadi ya wana-Kaya.

Hivyo basi, baada ya kuingia madarakani, Mzee Mwinyi alianzisha mageuzi makubwa ya kiuchumi, hususan kwa kuruhusu sekta binafsi kushirikiana na serikali katika kutoa huduma na kushiriki kwenye shughuli za kiuchumi. Sambamba na hayo, alianzisha ubinafsishaji wa mashirika ya umma, ambayo mengi yalikuwa yanaendeshwa kwa hasara na hivyo kuibebesha Serikali mzigo wa kuyahudumia. Miongoni mwa mashirika hayo ni Kiwanda cha Bia Tanzania. Mzee anaeleza kwenye Kitabu chake kuwa kabla ya kubinafsishwa, utendaji wa kiwanda hiki ulikuwa wa chini sana. Kwa mfano, ilikuwa ukitaka bia kwa ajili ya harusi, ilikulazimu kupata kibali cha kununua bia kutoka kiwandani au kwa wakala tena kwa kupeleka uthibitisho wa kadi za mialiko. Mbaya zaidi ni kwamba,

bia zilizokuwa zinazalishwa zilikuwa zinatofautiana viwango, unakuta bia moja ina kileo asilimia nne, nyingine saba, n.k. Aidha, haikuwa ajabu kukuta mzoga wa mende ndani ya chupa au kukuta inanuka mafuta ya taa. Mageuzi mengine aliyoanzisha Mzee Mwinyi ni katika sekta ya fedha na bima. Kwa ujumla, mageuzi haya yaliongeza ushindani na kuboresha upatikanaji wa huduma kwa wananchi.

Sambamba na mageuzi ya kiuchumi, Mzee Mwinyi ndiye aliyesimamia mageuzi makubwa ya kisiasa, hususan kurejesha Mfumo wa Siasa wa Vyama Vingi mwaka 1992. Hivyo basi, ni sahihi kusema kwamba Mzee Mwinyi ni Baba wa Mageuzi nchini.

Waheshimiwa Viongozi, Mabibi na Mabwana;

Mbali na mchango wake katika kusimamia mageuzi nchini, Kitabu cha Historia ya Mzee Mwinyi kinatufundisha mambo mengine mengi, hususan kwetu sisi viongozi. *Mosi*, Mzee Mwinyi ametufundisha kwamba, Uongozi wa nchi hautafutwi bali unatoka kwa Mungu. Kama mlivyosikia, Mzee Mwinyi alizaliwa Mkuranga, kisha wazazi wake wakampeleka Zanzibar ili kusoma dini kwa madhumuni ya kumtayarisha awe Sheikh Maarufu. Kama hiyo haitoshi, Mzee Mwinyi anaeleza kuwa hakuwa muasisi wa ASP na wala hakushiriki moja kwa moja kwenye Mapinduzi. Nafasi pekee kubwa aliyowahi kushika kwenye Chama ni Katibu wa ASP kwenye Tawi la Makadara, Zanzibar

Mjini. Pamoja na kwamba hakushika nafasi za juu katika chama cha ASP, kwa kudra na jaala ya Mwenyezi Mungu, aliweza kuwa Rais wa Zanzibar na hatimaye Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, tena bila kutumia nguvu wala kumuhonga mtu yeyote. Hili ni funzo kubwa sana kwa wote wenye dhamira ya kutaka kuwa viongozi wa nchi yetu, kwamba mbali na mikiki yetu tunaposaka madaraka, Uongozi wa jambo lolote lile ni kwa kudra, jaala na radhi za Mwenyezi Mungu.

Pili, Mzee Mwinyi ametufundisha kwamba, Uongozi ni dhamana. Kama tulivyosikia kutoka kwa Msoma Wasifu, mwaka 1977 wakati Mzee Mwinyi akiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi alijiuzulu nafasi yake

kwa hiari kufuatia mauaji yaliyotokea wakati wa mahojiano na watuhumiwa wa mauaji ya vikongwe Shinyanga kwa imani ya ushirikina. Hili ni fundisho kubwa sana kwetu sisi viongozi wa sasa.

Tatu, Kitabu cha Mzee Mwinyi kinatufundisha kuwa Uongozi sio lelemama. Ukikubali kuwa Kiongozi ujue ni lazima utakumbana na changamoto mbalimbali. Mbali na matatizo ya kiuchumi aliyokumbana nayo, Mzee Mwinyi anakumbuka changamoto nyingine alizokumbana nazo wakati wa uongozi wake, ikiwemo kuibuka kwa ugonjwa wa UKIMWI, migomo ya wanafunzi na wafanyakazi; migogoro ya kidini, kuibuka kwa kundi la G-55, n.k. Silaha pekee iliyompa ujasiri na nguvu ya kuendelea na Uongozi, ni Uvumilivu na Ustahamilivu.

Funzo la *nne* kubwa ambalo tunalipata kwenye Kitabu cha Mzee Mwinyi ni umuhimu wa kukiri makosa. Viongozi sio malaika, viongozi ni binadamu; na binadamu kwa kawaida ameumbiwa kufanya makosa. Mzee Mwinyi anakiri kwamba katika kipindi chake cha Uongozi yalifanyika baadhi ya makosa. Mathalan, kwenye ukurasa wa 233 - 234, anazungumzia baadhi ya makosa yaliyofanyika wakati wa kufanya mageuzi ya kiuchumi kwa kusema kuwa *“ukifungua madirisha kuruhusu hewa safi kuingia ndani ya nyumba, aghalabu na nzi, mbu na vumbi huweza kuingia”*. Anatoa mfano wa namna misamaha ya kodi iliyotolewa ili kuvutia uwekezaji na biashara ilivyotumika vibaya na baadhi ya wajanja.

Tano, Mzee Mwinyi anatufundisha umuhimu wa sisi binadamu, hususan viongozi kupendana na kushirikiana. Kama tulivyosikia, mwaka 1981, Mzee Mwinyi aliteuliwa kuwa Waziri wa Nchi alipoanzia Ofisi ya Rais (Muungano). Kabla ya uteuzi alikuwa anaishi nyumba ya serikali Osterbay na wakati huo alikuwa akijenga nyumba yake hapo Mikocheni; na vifaa vyake vya ujenzi aliviweka kwenye nyumba hiyo ya Serikali. Hivyo, baada ya uteuzi wa mwaka 1981, alitakiwa kuhama kwenye nyumba ya Osterbay, ambayo ilipangiwa kukaa Waziri mwingine. Mzee Mwinyi anasema Waziri mpya alikuja nyumbani na kumtaka aondoke haraka hata bila ya kumpa nafasi ya kuhamisha vitu vyake vya ujenzi.

Mzee Mwinyi alikubali kuondoka na kuacha vifaa vyake kwenye nyumba hiyo. Baada ya kuchaguliwa kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, pamoja na kufanyiwa vitimbwi hivyo, Mzee Mwinyi alimteua Waziri huyo kwenye Baraza lake la Mawaziri. Sina hakika, wangapi kati yetu tungeweza kufanya hivyo. Na hapa tunapata fundisho jingine kuwa sisi binadamu hatuna budi kuspendana, kuheshimiana, kuacha kudharauliana, kwani unayemfanyia vitimbi leo, hujui kesho mtakutana wapi, akiwa nani. Vilevile, ametufunza kutokuishi na visasi miongoni mwetu.

Waheshimiwa Viongozi;

Wageni Waalikwa, Mabibi na Mabwana;

Leo sio siku ya hotuba. Tupo hapa kwa ajili ya kuzindua Kitabu cha Mzee Mwinyi, Mtanzania pekee, ambaye amebahatika kuwa Rais wa Zanzibar na pia Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mpaka sasa. Alhamdulillah. Hivyo basi, baada ya shukurani kwa Mwenyezi Mungu, narudia kumshukuru sana Mzee wetu Mwinyi kwa kuandika Kitabu hiki ambacho mbali na kumtambulisha vilivyo yeye binafsi, ni kati ya vitabu vyengine vinavyotupa fursa ya kujifunza mienendo ya maisha, changamoto, hulka na mafanikio ya wengine, mambo ambayo yanatupa mifano ya mienendo ya kuiga au kujifunza. Hii ni ishara ya mapenzi makubwa aliyonayo kwetu Watanzania. Hatuna budi tukitafute na kukisoma kitabu hiki, ambacho kina hazina kubwa ya mambo ya kujifunza kwa kizazi cha sasa na kijacho.

Mbali na mafunzo yaliyomo, ndani ya Kitabu hiki kuna hadithi nyingi za kuisisimua kumhusu Mzee Mwinyi na nchi yetu kwa ujumla. Ukisoma Kitabu hiki utafahamu pia historia ya majina kama Namanga hapa Dar es Salaam na pia Mangapwani kule Zanzibar.

Napenda pia kutumia fursa hii kuishukuru na kuipongeza Taasisi ya Uongozi, ambayo imeshirikiana na Mzee Mwinyi katika kukiandaa kitabu, na naishukuru Kampuni ya Mkuki na Nyota kwa kuchapisha Kitabu hiki. Kwa namna ya pekee, naishukuru Serikali ya Finland, ambayo tangu kuanzishwa kwa Taasisi ya Uongozi mwaka 2010, imekuwa ikitoa msaada wa fedha na ushauri. Tunawashukuru sana rafiki zetu wa Finland, ambao

tunashirikiana nao pia kwenye masuala mengine, ikiwemo kwenye sekta za misitu, elimu, TEHAMA, n.k. Kwenye hotuba ya Mwakilishi wa Ubalozi wa Finland ameomba kuundwa kwa Bodi ya Taasisi ya Uongozi na ameniomba tushirikiane nao katika kuendesha mafunzo ya uongozi kwa wanawake. Nataka nimhakikishie kuwa Wajumbe wa Bodi hiyo watateuliwa hivi karibuni; aidha, tupo tayari kushirikiana nao katika kutoa mafunzo ya Uongozi kwa Wanawake. Kama usemi wa Kiswahili usemavyo *“Ukimwelimisha mwanamke, umeielimisha jamii”*.

Mheshimiwa Mzee Mwinyi;

Waheshimiwa Viongozi;

Wageni Waalikwa, Mabibi na Mabwana;

Nihitimishe kwa kuwashukuru wageni wenzangu wote waalikwa mliohudhuria Hafla hii. Nimefurahi kuwaona Viongozi wengi, wakiwemo wastaafu, wameshiriki kwenye Hafla hii. Namuona Rais Mstaafu wa Awamu ya Nne, Mhe. Kikwete, ambaye kwa taarifa nilizonazo naye yupo kwenye hatua za mwisho za kukamilisha Kitabu cha Historia ya Maisha yake. Ni matumaini yangu kwamba, atakapokikamilisha, tutapata fursa kama hii ya kukizindua Kitabu chake.

Baada ya kusema hayo, sasa nipo tayari kutekeleza jukumu lililonileta hapa la kuzindua Kitabu cha Maisha ya Mheshimiwa Mzee Mwinyi « *Mzee Rukhsa: Safari ya Maisha Yangu* ». Kabla sijafanya hivyo, kama mnavyojua leo ni siku ya kuzaliwa kwa Mzee wetu, siku kama leo

waalikwa hutoa zawadi kwa mzaliwa. Nimemuangalia Mzee Mwinyi Umri 96 leo, Kimo chake na usumbufu anaoupata wakati wa kupanda au kushuka kwenye gari anayoitumia, nimeona tumpunguzie kadhia hiyo, na kwa niaba ya Serikali, tumeamua kumpatia Mzee wetu gari itakayompa raha katika safari zake.

Mungu Mbariki Mzee Mwinyi na Familia yake!

Mungu Ibariki Tanzania!

**Nawasalimu tena kwa Jina la Jamhuri ya Muungano wa
Tanzania**

« Ahsanteni sana kwa kunisikiliza »